# UMAHIRI WA MSINGI

IAF kwa Kiingereza, “International Association of Facilitators” ni chama cha kimataifa cha wawezeshaji kilichoanzishwa kwa lengo la kuhamasisha na kuendeleza taaluma ya uwezeshaji kwa kubuni na kuibua njia mbalimbali za kuwezesha vikundi kupanga na kufanya maamuzi shirikishi kwa ufanisi na ukamilifu.

Kihunzi (Framework) cha kwanza cha Umahiri wa Msingi kiliandaliwa na IAF kwa lugha ya kiingereza miaka ishirini iliyopita na imefanyiwa marudio mwaka wa 2003 na 2021. Makala ya Kiswahili ilitolewa mwaka 2015. Makala hii ya 2022 inabeba maboresho yaliyofanyika mwaka 2021 katika ile Makala ya Kiingereza. Mbali na lugha ya Kiingereza na Kiswahili, IAF imetoa makala za “Umahiri wa Msingi katika lugha nyingine tisa; Kiarabu, Kifaransa, Kiitaliano, Kijapani, Kichina (Mandarin), Kiajemi (Persian) Kireno, Kirusi na Kihispania. Makala hizi katika lugha.

Mwezeshaji mahiri anatakiwa kuwa na muungano wa ujuzi unaoleta pamoja stadi, maarifa na tabia ambazo huchangia kumfanya awe na uwezo wa kufanya kazi katika mazingira tofauti kiufanisi.

Hizi Umahiri wa Msingi za IAF, kanuni za maadili na tamko la tunu zake ndiyo uti wa mgongo wa kazi, programu na tuzo za IAF ambazo zinapatikana katika tovuti ya IAF: IAF Facilitation Impact Award, IAF Mentoring Programme, IAF Endorsed™ Facilitator, IAF Certified, Professional™ Facilitator, IAF Certified™ Professional Facilitator | Master and IAF Certified™ Professional Facilitator | Emeritus, IAF, Endorsed™ Facilitation Training Programmes.

Ukihitaji msaada zaidi unapatikana kwa lugha ya kiingereza kwenye: certification@iaf-world.org

Toleo hili la Kiswahili la 2022 limeandaliwa na timu ya wanachama wa IAF – Tanzania ikiongozwa na Dr. Aichi J. Kitalyi Mratibu

promoting the power
of facilitation worldwide

| A. JENGA UHUSIANO UNAOLETA USHIRIKIANO BAINA YAKO NA MTEJA[1] |
|---|
| **1. Dumisha uhusiano shirikishi wa utendaji** |
| • Fafanua dhamira na uwajibikaji wa pamoja |
| • Jenga makubaliano kuhusiana na kazi inayopaswa kufanyika, nini kinatarajiwa kupatikana mwisho wa kazi, majukumu na wajibu |
| • Onesha thamani au nguvu ya ushirikiano na mchakato |
| **2. Unda na rekebisha malengo ili kuendana na mahitaji ya mteja** |
| • Changanua mazingira ya kiasasi |
| • Chunguza mahitaji ya mteja |
| • Ibua majukumu ya wadau na kiwango cha ushiriki wao |
| • Buni njia fanisi za kufikia matokeo yanayotarajiwa |
| • Fafanua kiwango cha ubora wa matokeo tarajiwa na mteja |
| **3. Simamia na kuongoza matukio ya vipindi mbalimbali  kwa ufanisi** |
| • Ingia mkataba na mteja unaoonyesha upeo wa kazi na matokeo |
| • Tengeneza mpango wauendeshaji wa tukio husika |
| • Kamilisha tukio kikamilifu |
| • Tathimini kuridhika kwa mteja katika hatua zote za tukio au mradi |

[1] Mteja: Mteja Anafasiriwa kama asasi, kikundi ama mtu ambaye anapewa kazi namwezeshaji

## B. PANGA MCHAKATO KIKUNDI MUAFAKA

### 1. Chagua mbinu sahihi na mchakato uutakao:

- Himiza ushiriki wa wazi unaojali tamaduni za mteja, desturi na uanuai wa washiriki
- Husisha washiriki wenye mbinu mbali mbali za mafunzo na njia za kuchambua taarifa
- Hakikisha unapata matokeo bora yenye viwango yanayoendana na mahitaji ya mteja

### 2. Tenga muda na nafasi ya kutosha kuwezesha mchakato wa kikundi

- Panga nafasi sahihi na utaratibu wa kuwezesha shughuli za mkutano
- Panga kikamilifu matumizi ya muda
- Weka mazingira mazuri na yenye kusaidia madhumuni ya vipindi / mikutano

## C. JENGA NA ENDELEZA MAZINGIRA SHIRIKISHI

### 1. Onesha kwa vitendo ushirikishwaji kamilifu na stadi fanisi za mawasiliano baina ya watu

- Tumia mbinu mbalimbali za michakato shirikishi
- Onesha kwa vitendo stadi fanisi za mawasiliano ya kuzungumza
- Jenga maelewano ya karibu na washiriki
- Kuwa makini na msikivu
- Onesha uwezo wa kuchunguza na kutoa mrejesho kwa washiriki

| 2. Heshimu na tambua uanuai kwa kuzingatia ujumuishi |
|---|
| • Himiza washiriki kuchangia uzoefu na fikra chanya kwa wote |
| • Jenga mazingira ya kuminiana na salama |
| • Tambua vikwazo kwa washiriki na njia za kuondoa vikwazo hivyo |
| • Pokea na kuyakubali mawazo yote bila kuyatolea hukumu |
| • Ibua furusa kwa washiriki kunufaika na uanuai uliopo katika kikundi. |
| • Jenga ufahamu wa kitamaduni na unyeti wake |
| **3. Simamia na dhibiti migogoro ya Kikundi** |
| • Wasaidie washiriki kupitia na kutambua mambo yanayosababisha migogoro |
| • Tambua migogoro na nafasi yake katika ujifunzaji wa Kikundi/ukomavu |
| • Weka mazingira salama yatakayozuia migogoro kuibuka |
| • Dhibiti tabia mbalimbali zinazojitokeza miongoni mwa washiriki zinazochangia kutokea kwa migogoro |
| • Tambua na dhibiti misongo na migogoro na athari zake katika kufikia uamuzi wa Kikundi wa pamoja |
| • Uwe makini na sababu za kitamaduni kuhusiana na migogoro |
| **4. Amsha ubunifu wa Kikundi** |
| • Cokonoa washiriki kwa kutumia mbinu mbali za mafunzo na njia ya kuchakata taarifa |
| • Himiza fikra bunifu/tunduizi |
| • Tumia mbinu muafaka zinazokidhi mahitaji na uwezo wa Kikundi |

| |
|---|
| • Chochea na tumia uwezo na nguvu ya kikundi |

| **D. ONGOZA KiKUNDI ILI KUFIKIA MATOKEO TARAJIWA NA YENYE MSHIKO/MANUFAA** |
|---|
| **1. Ongoza Kikundi kwa kutumia mchakato na mbinu za kueleweka** |
| • Tengeneza muktadha uliowazi kwa kila kipindi |
| • Fafanua na na toa muhtasari kupata hisia na fikra za Kikundi |
| • Ongoza mchakato wa kikundi kidogo na kikubwa |
| **2. Wezesha Kikundi kujitambua kuhusiana na kazi/shughuli yao** |
| • Rekebisha kasi ya shughuli kulingana na mahitaji ya Kikundi |
| • Tambua ni taarifa gania mbazo zinahitajika kwa Kikundi, chukuwa data na utambuzi wao kutoka kwenye Kikundi |
| • Saidia Kikundi kuweza kuunganisha taarifa, visababishi, nakujengampangowakuchukuahatua. |
| • Saidia Kikundi kuelewa undani wa majadiliano, fafanua mifumo, mwelekeo, visababishi msingi, na utaratibu wa utekelezaji . |
| **3. Ongoza Kikundi ili kuweza kufikia muafaka na kupata matokeo tarajiwa** |
| • Tumia mbinu anuai ili kufikia maridhiano ya Kikundi |
| • Tumia mbinu anuai ili kufikia malengo ya Kikundi |
| • Kubaliana na michakato kulingana na hali ya mabadiliko na mahitaji ya Kikundi |
| • Pima na wasiliana maendeleo ya Kikundi |
| • Tambua na fafanua mielekeo sahihi ili kubadili mitazamo/kuangalia upya shuguli/kazi |

| |
|---|
| • Himiza kukamilisha kazi kwa wakati |

| |
|---|
| **E. JENGA NA ENDELEZA UFAHAMU WA KITAALAMU** |
| **1. Endeleza uwanja mpana wa maarifa** |
| • Uwe na ufahamu katika nadharia na vitendo juu ya mchakato wa uwezeshaji wa Kikundi na maarifa yanayolandana yanayohusu watu, asasi, vikundi na michakato (mfano ukuaji wa asasi, elimu nafsia (saikolojia), utatuzi wa migogoro, mienendo ya mabadiliko, ujifunzaji, na nadharia ya kufikiri) |
| **2. Fahamu mbinu mbalimbali za uwezeshaji** |
| • Elewa modeli mbalimbali na michakato inayosaidia vikundi kuibua mawaidha, kutatua matatizo, kuweka vipaumbele, kupanga, na kufanya maamuzi. |
| • Elewa mbinu na stadi anuai za kikundi. |
| • Fahamu madhara ya matumizi mabaya ya mbinu za kikundi (Group methods) |
| • Tofautisha michakato baina ya shughuli/kazi na maudhui |
| • Jifunze michakato, njia, modeli, na tekinolojia mpya katika kusaidia mabadiliko ya mteja/mahitaji yanyojitokeza |
| **3. Dumisha misimamo ya kitaaluma** |
| • Kuwa na mafunzo endelevu katika fani ya uwezeshaji |
| • Endelea kupata uelewa na ufahamu endelevu na taarifa mpya kuhusiana na taaluma yetu ya uwezeshaji |
| • Jizoeshe kufanya tafakuri na kujifunza |
| • Jijengee ujuzi/ufahamu binafsi na mitandao katika maeneo ya fani yetu. |

promoting the power
of facilitation worldwide

| F. KUWA NA MITAZAMO CHANYA KITAALUMA KAMA MWEZESHAJI WA MICHAKATO |
| --- |
| **1. Jenga tabia ya kufanya tathmini binafsi na kujitambua** |
| • Fanya tafakuri kuhusu tabia na matokeo ya jumla |
| • Dumisha uwiano mzuri kati ya matendo na maadili binafsi na maadili ya kitaaluma |
| • Rekebisha tabia binafsi, na mitindo yako ya maisha kuendeana na mahitaji ya kikundi |
| • Jenga uwelewa wa maadili wa mtu binafsi na athari zake katika kufanya kazi na wateja |
| **2. Onesha uadilifu** |
| • Onesha kwa vitendo imani yako kwa kikundi na yanayowezekana. |
| • Kabili hali mbalimbali kwa uhalisia na ukiwa na mitazamo chanya |
| • Kama mwezeshaji, fafanua hali mbalimbali kwa jinsi unavyoziona na ulizia mitizamo tofauti |
| • Onesha mipaka ya kitaaluma na maadili (kama ilivyoainishwa katikaTaarifa ya Maadili ya IAF na Kanuni za Maadili) |
| **3. Amini uwezo wa Kikundi na mfano wa kutoegemea upande wowote (Neutrality)** |
| • Tambua, thamini, na heshimu hekima ya Kikundi |
| • Himiza uaminifu katika uwezo na uzoefu wa wengine |
| • Kuwa makini katika Kushawishi mwelekeo wa majadiliano na matokeo ya Kikundi.Simamia malengo sahihi na msimamo usio wa kujihami, na usio wa kukosoa au kuhukumu |